**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SITA**

**Kikao cha Kwanza - Tarehe 30 Januari, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wengi walikuwa nje. Nisuburi kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba mwanzoni mwa mwezi huu tumepata msiba mkubwa katika Bunge hili kwa kupotelewa na mwenzetu aliyekuwa Mbunge wa Tunduru na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Masuala ya Bunge, Mheshimiwa Juma J. Akukweti. Kama ilivyo kawaida, kwa heshima yake tusimame kimya kwa dakika moja.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walisimama kwa dakika moja)*

**SPIKA:** Ahsante. Tukae! Namwomba Mwenyezi Mungu mwenye rehema kuu ailaze roho ya Marehemu Akukweti mahali pema Peponi. Amin.

**TAARIFA ZA SPIKA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, taarifa ya msiba nimekwishatangaza. Naomba kutoa taarifa kwamba Miswada ifuatayo ambayo ilipitishwa na Bunge katika Mkutano wake wa Tano, imekwishapata kibali cha Mheshimiwa Rais na sasa ni Sheria za nchi yetu kama ifuatavyo:-

(i) *The Written Laws Miscellaneous Amendments Act, 2006* Na. 8 ya mwaka 2006;

(ii) *The Local Authorities Pensions Fund Act, 2006* yaani Na. 9 wa mwaka 2006;

(iii) *The Meat Industry Act, 2006*, Sheria Na. 10, 2006;

(iv) *The Universal Communications Service Access Act, 2006* yaani Na. 11 ya Mwaka 2006;

(v) *Anti-Money Laundering Act, 2006* Na. 12 wa 2006; na

(v) *The Local Government Laws Miscellaneous Amendment Act, 2006* yaani Sheria Na. 13 ya 2006.

## HATI ILIYOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI:**

Taarifa ya Matoleo yote ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake zilizochapishwa tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita.

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, swali la kwanza linaelekezwa Ofisi ya Waziri Mkuu na linaulizwa na Mheshimiwa Clemence B. Lyamba. Kabla halijajibiwa, ninataka tu nimpongeze Mheshimiwa Dr. Buriani kwa sababu sina hakika pengine anaweza kutaka kusimama kwa nyongeza.

Kwa hiyo, ni vizuri nimpongeze kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Shughuli za Bunge. *(Makofi)*

Tunampongeza sana! Tuna imani kwamba jinsi ambavyo ameihudumia nchi yetu hadi sasa kwa uadilifu na kwa bidii, atatumia vipaji hivyo hivyo kuendeleza nchi yetu katika wadhifa huo.

Na.1

### Hitaji la Kituo cha Elimu Juu ya UKIMWI - Mikumi

**MHE. ABBAS ZUBERI MTEMVU (K.n.y. MHE. CLEMENCE B. LYAMBA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Kijiji cha Mikumi kina maumbile na tabia ya Mji mdogo kama ilivyo Chalinze na kwa kuwa pia ni njia panda kubwa katika barabara kuu itokayo Morogoro kuelekea Iringa, Mbeya, Tunduma, Zambia hadi Afrika Kusini na tena ni makutano ya barabara zitokazo Ifakara hadi Mahenge upande wa kusini na barabara itokayo Kilosa hadi Dumila upande wa kaskazini hali inayosababisha mkusanyiko wa watu wakati wote na kwa kuwa baada ya safari ndefu kutoka kila upande, Mikumi ni kituo kikubwa chenye mandhari inayovutia kupumzika na kujiliwaza kwa madereva wengi wa magari ya mizigo na abiria na pia ni sehemu yenye mvuto wa burudani zinazokusanya wafanyakazi wengi

kutoka Taasisi jirani kama Kampuni ya Sukari Kilombero, *TANESCO* – Kidatu, *VETA* – Mikumi pamoja na Watalii kutoka Hifadhi ya Wanyama ya Mikumi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kitaifa wa kuanzisha kituo chini ya *TACAIDS* kitakachotoa uenezi wa elimu juu ya UKIMWI na uhamasishaji madhubuti wa kujikinga na ugonjwa huo katika eneo hilo dogo lenye watu wengi kupita kiasi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Mikumi ina sifa na vivutio mbalimbali, lakini vile vile ni eneo mojawapo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa ambapo kasi ya maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI ni zaidi ya asilimia saba (7%) kwa mwaka kufuatana na Takwimu za Hospitali ya Wilaya ya Kilosa kwa mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Kilosa ni miongozi mwa Halmashauri 22 nchini ambazo zinatekeleza programu inayofadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa kupambana na ugonjwa wa Malaria, Kifua Kikuu na UKIMWI *(Global Fund Round Four)*. Aidha, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Halmashauri hiyo ilipata kiasi cha Sh. 263,463,673/= kwa ajili ya kutekeleza kazi ziofuatazo:-

- Kutoa mafunzo kwa jamii juu ya umuhimu wa kupima afya zao;
- Kujenga vituo vya kupima na kutolea ushauri nasaha;
- Kutoa dawa za kupunguza makali ya UKIMWI; na
- Kuhudumia wagonjwa wa UKIMWI majumbani *(Home Based Care).*

Mheshimiwa Spika, fedha ambazo zimetumika hadi Desemba, 2006 ni Sh. 102,033,000/= kwa ajili ya kujenga uwezo wa kudhibiti maambukizi ya UKIMWI kwa Wilaya nzima ya Kilosa. Kwa upande wa Mikumi, kazi zifuatazo zimefanyika:-

- Vituo vitatu vya upimaji na ushauri nasaha vimeanzishwa. Kuna Kituo cha Afya Kilombero II, Kituo cha Afya Kidodi na Kituo cha Afya Mikumi;
- Jumla ya watu 1,055 walipimwa afya zao katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2006;
- Vijana 36 kutoka Kata zote za Tarafa ya Mikumi wamepatiwa mafunzo ya uelimishaji juu ya magonjwa ya ngono na UKIMWI;

- Kuzuia maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto; na

- Wananchi 44,256 wamefikiwa na uelimishaji juu ya kinga dhidi ya UKIMWI kuanzia Septemba hadi Novemba, 2006.

Mheshimiwa Spika, katika Mji mdogo wa Mikumi kipo Kituo cha Afya chini ya Kanisa Katoliki ambacho kinatoa huduma za elimu, upimaji na ushauri nasaha kuhusu udhibiti wa maambukizi ya UKIMWI. Kwa mwaka 2007/2008, Halmashauri ina mpango wa kupanua Zahanati ya Mikumi ili iweze kutoa huduma hizo za kuzuia maambukizi ya UKIMWI. Kiasi cha Sh. 101,000,000/= kutoka *Global Fund* zinatarajiwa kutumika kwa kazi hizo kwa Wilaya nzima ya Kilosa.

Na.2

**Ushiriki wa Wanawake katika Mipango ya Maendeleo**

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA** aliuliza:-

Kwa kuwa, ushiriki wa wanawake katika mipango ya maendeleo na vikao vya *WDC* ni jambo muhimu sana hasa katika ngazi za chini, yaani Vijiji na Vitongoji na kwa kuwa Wajumbe halali wa *WDC* ni Wenyeviti wa Mitaa na kwa kuwa Kata nyingi hazina Wenyeviti wa Mitaa wanawake:-

(a) Je, mawazo ya wanawake yanawasilishwa na nani katika *WDC* zenye wanaume tu?

(b) Je, Serikali haioni kuwa inawanyima wanawake haki ya kushiriki katika ngazi ya Kata na badala yake kuendeleza mfumo dume?

(c) Je, ni kwa nini mfumo wa asilimia thelathini (30%) hautumiki katika ngazi ya Wenyeviti wa Mitaa kama ilivyo kwa Wabunge na Madiwani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Devota Likokola, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a), (b) na (c), naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, muundo wa Wajumbe wa Kamati za Maendeleo ya Kata *(WDC)* umeelezwa katika kifungu cha 31(2) cha Sheria Na. 7 ya mwaka 1982 kwa Mamlaka za Wilaya na kifungu cha 15(2) cha Sheria Na. 8 ya 1982 kwa Mamlaka za Miji. Katika Muundo huo, Mwenyekiti wa *WDC* ni Diwani anayewakilisha Kata husika na Mtendaji wa Kata ni Katibu. Aidha, Wajumbe wengine ni Wenyeviti wa Vijiji/Mitaa, Madiwani wa kuteuliwa wanaoishi katika eneo hilo na watu wengine wanaoweza kualikwa na Kamati lakini hawana haki ya kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, aidha, kifungu cha 14(a)(i) cha Sheria Na. 8 ya mwaka 1982 kimeeleza muundo wa Kamati ya Mtaa. Sheria hiyo inatamka pia kwamba Kamati ya Mtaa itakuwa na Wajumbe sita. Wawili kati yao lazima wawe wanawake. Serikali ya Kijiji inaundwa na Mwenyekiti wa Kijiji, Wenyeviti wa Vitongoji, Wajumbe wa kuchaguliwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji.

Kwa mujibu wa Sheria hiyo, idadi ya Wajumbe wa Serikali ya Kijiji ni kati ya 15 – 25 ambao theluthi moja ya Wajumbe hao lazima wawe wanawake. Maamuzi ya msingi ya kimaendeleo hufanyika kwenye ngazi ya Kijiji na Mtaa. Ngazi hizi zinawakilishwa na wanawake kwa asilimia zaidi ya thelathini. Aidha, *WDC* ina jukumu la kuratibu na kuwezesha na sio kubadilisha maamuzi ya ngazi za Kijiji.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Devota Likokola, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Wajumbe halali wa *WDC* ni Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa. Mawazo ya wanawake yanawasilishwa kwenye Kamati ya *WDC* kutoka kwenye Mkutano Mkuu wa Kijiji au wa Mtaa unaofanyika mara nne kwa mwaka ambao kila mtu anaalikwa kuhudhuria na kutoa mawazo yake ikiwa ni pamoja na wanawake. Muafaka ambao utafikiwa na wananchi walio wengi ndio utakaowasilishwa kwenye Kamati ya Maendeleo ya Kata *(WDC)*. Jambo muhimu ni kwa wanawake kujitokeza kwa wingi na kuhudhuria Vikao/Mikutano ya Vijiji au mitaa na vile vile kugombea nafasi mbali mbali za uongozi katika ngazi hizo.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali haijawanyima haki wanawake kushiriki katika ngazi ya Kata. Wanawake wamekuwa wakihamasishwa kujitokeza na kugombea nafasi mbalimbali za uongozi. Aidha, katika ngazi ya Kata ukiondoa Wajumbe waliotajwa kisheria, washiriki wengine ni wataalam walioalikwa ili kutoa ufafanuzi katika majadiliano mbali mbali. Hivyo, ngazi hii ni ya utaratibu na uwezeshaji zaidi kuliko uwakilishi wa kuteuliwa.

(c) Mheshimiwa Spika, mfumo wa demokrasia uliopo katika malmlaka za Serikali za Mitaa unatoa uwakilishi wa theluthi moja ya wajumbe sawa na asilimia 33.3% kwa wanawake katika ngazi za Vijiji na Mitaa ambao ni kiwango kikubwa kuliko uwakilishi wa asilimia thelathini (30%) unaotumika kwa Wabunge na Madiwani.

Napenda kutoa wito kwa wanawake kujitokeza na kugombea nafasi mbali mbali za uongozi ili mawazo yetu yaweze kuwakilishwa ipasavyo.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru pia kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ameyatoa.

Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza Mfumo ambao unatumika kwenye *WDC,* ni kwamba, una uwakilishi maalum na wanawake. Lakini katika hali halisi ya kwenye *WDC*

zetu, nafikiri wote tunafahamu uwakilishi wa wananwake ni hafifu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri anasema nini kutokana na hali hiyo halisi iliyoko kwenye *WDC* zetu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ninaomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, kwa kuwa mimi na wanawake wengi Tanzania tunaamini kwamba kuna wanawake wenye sifa, vigezo na uwezo wa kushika nyadhifa mbali mbali za kiutendaji na maamuzi na kwa vile sasa hivi hilo limethibitishwa na Umoja wa Mataifa kwa kumteua Dr. Asha-Rose Migiro; Je, Serikali sasa iko tayari kuteua wanawake wengi katika vyombo vya utendaji na maamuzi kama vile Wakuu wa Mikoa, Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri, Makatibu Wakuu ambao idadi yao ni ndogo sana sasa hivi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Naona swali limepanuka hadi kufikia ngazi ya Taifa, uwakilishi katika Taifa. Limeanzia Vijiji. Lakini pengine Mheshimiwa Naibu Waziri utapenda tu kujibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu uwakilishi hafifu kwenye *WDC* kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba *WDC* Wawakilishi halisi ambao wanatoa maamuzi ni kutoka katika ngazi ya Vijiji na ngazi ya Mitaa. Kule ndiko wanakoamua kwamba nini kifanyike katika Kijiji chetu au ni nini kifanyike katika Mtaa wetu. Likiingia kwenye *WDC*, wao ni kubariki na kuiweka vizuri ili irudi kwenye utendaji, kwa hiyo, uwakilishi ule ambao Serikali imeweka kwenye sheria kwamba theluthi ya Wajumbe katika Kijiji au Mtaa wawe wanawake ni uwakilishi tosha kwa sisi wanawake katika maamuzi mbali mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kitaifa, nafikiri tungeipongeza Serikali kwa sasa hivi, Serikali ya Awamu ya Nne kwa mchango mkubwa kwa upande wa wanawake. Mathalani, naomba kutoa mifano michache tu ambayo Serikali imewateua wanawake katika nyadhifa mbalimbali.

Tukianzia katika ngazi ya Mawaziri, asilimia 30 ya Mawaziri ni wanawake; tukienda kwenye Manaibu Waziri, asilimia 33 ni wanawake; tukishuka kwenye ngazi ya Makatibu Wakuu, angalau asilimia kati ya 20 – 30 ni wanawake; kwa ma-*RC* ni ndogo, lakini wapo angalau watatu. Juzi juzi Serikali imeteua Majaji. Kati ya Majaji 20, saba ni wanawake. Jamani hiyo hatua lazima tuipongeze pia! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wakuu wa Wilaya, nafikiri ni mfano tosha kwamba asilimia 50 ni wanawake na kwa Upande wa Wakurugenzi, kadhalika ni kati ya asilimia 20 – 30.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali ina moyo wa kutujali na itazidi kutujali na kuongeza nafasi mbalimbali hasa kwa wale wenye sifa na uwezo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani limetosheleza! Kabla sijamwita mwuliza swali linalofuata ambalo linaelekezwa Wizara ya Miundombinu, sio kawaida yangu sana, lakini napenda kumpongeza sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Celine Kombani, kwa sababu kidogo nikatae swali la pili la nyongeza kwa kuwa lilitoka kwenye Vijiji na *WDC* likaenda ngazi ya Taifa.

Kumbe kutokana na maandalizi mazuri ya majibu, Mheshimiwa Celine Kombani alifikiria yote mpaka lingeulizwa la Taifa ingekuwa vipi! Bahati njema yeye ni mwanamke na niseme tu mimi ni mzee, namtabiria mambo mema siku za usoni. *(Kicheko/Makofi)*

Na. 3

**Barabara ya Kutoka Tabora – Nzega na Kahama**

**MHE. TEDDY L. KASELA-BANTU** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais Kikwete alipopita katika Jimbo la Bukene wakati wa Kampeni za Uchaguzi aliahidi kwamba, barabara ya kutoka Tabora kwenda Nzega kupitia Maambali – Bukene – Itoba na Itoba – Igusule kwenda Kahama kuwa itatengenezwa kwa kiwango cha changarawe:-

(a) Je, ni lini barabara hiyo itashughulikiwa?

(b) Kwa kuwa ahadi ni deni, hasa inapotolewa na Mheshimiwa Rais, ahadi zake huwa za papo kwa papo na wala haionekani katika ahadi/mipango ya utekelezaji ya Mkoa wa Tabora; Je, kazi hiyo itafanyika lini?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mbunge wa Bukene, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Tabora – Mambali – Bukene hadi Itobo yenye jumla ya kilometa 120 ni barabara ya Mkoa. Barabara ya kutoka Nzega – Itobo hadi Bukoba mpakani na Kahama yenye jumla ya kilometa 55 ni barabara kuu, ingawa inafikiriwa kushushwa daraja kuwa barabara ya Mkoa baada ya kukamilishwa ujenzi wa barabara ya Nzega –Tinde – Isaka. Barabara hizo zote zinaruhudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka huu wa fedha 2006/2007, kipande cha barabara kutoka Tabora hadi Mambali kilometa 54.2 kinafanyiwa ukarabati wa kiwango cha changarawe chini ya ufadhili wa *NORAD* kwa gharama ya Shilingi bilioni 1,139.89. Kazi za ukarabati zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2007.

Aidha, katika mwaka huu wa fedha 2006/2007 kipande cha kutoka Mambali – Bukene – Itobo kilometa 58.5, kitaendelea kufanyiwa matengenezo ili kiweze kuendelea kupitika wakati wote. Kiasi cha Shilingi milioni 35 kimetengwa kwa ajili ya kugharamia matengenezo maalum *(periodic maintenance)* na Shilingi milioni 40 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida *(routine maintenance).*

Mheshimiwa Spika, kipande cha barabara Kuu kutoka Nzega – Itobo hadi Bukoba mpakani na Kahama kilometa 55, kitaendelea kufanyiwa matengenezo na kiasi cha Shilingi milioni 57 kimetengwa katika mwaka huu wa fedha 2006/2007 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kufanyia ukarabati kwa kiwango cha changarawe barabara hizo kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuongeza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa alipokuwa anapita kuangalia barabara hiyo niliyoitaja, Mheshimiwa Naibu Waziri na mimi nikiwa naye, tulipofika Mambali, wananchi walimwambia barabara ile ya *Old Mwanza* inayotoka Tabora kwenda Mwanza ambayo ni ya historia kutoka Wajerumani, waliiomba barabara hiyo. Hiyo inatokana na barabara, yaani inatakiwa kuhudumiwa na *TANROADS* kwa sababu inatoka Mkoa wa Tabora, inaingia Mkoa wa Shinyanga na inakwenda mpka Mkoa wa Mwanza.

Mheshimiwa Spika, barabara hiyo ambayo inapita katika Jimbo langu na la wakulima wengi zaidi wa Kata ya Semembela, Kamayahalanga, Ikindwa, Malolo pale pamoja na Mwamalwa kutokea Igusule kwenda Kahama na kuunga kwenda Bukoba na kuunga kwenda Mwanza ili kuwasaidia wakulima hawa kupeleka mazao yao sokoni; Je, Serikali inasemaje kuwasaidia ili waweze kutoa mazao yao katika sehemu hizo nilizozitaja kupeleka mazao sokoni?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli mimi na yeye tulitembelea barabara hiyo na alitoa kauli hiyo au maombi hayo kwamba barabara ambayo zamani ilikuwa inajulikana kama *Old Mwanza* ile ya kutoka Mambali kuelekea Mkoa wa Shinyanga iweze kupandishwa hadhi, ishughulikiwe na *TANROADS*. Lakini mimi na yeye tulikwenda mpaka Wilayani tukazungumza na viongozi wa Wilaya ya Nzega na tukagundua kwamba hii barabara iliishashushwa daraja na kwa kweli sasa wala siyo barabara ya Wilaya, ni barabara ya Kijiji.

Mheshimiwa Spika, sasa, naomba ushauri wangu niliotoa kwa Injinia wa Wilaya ya Nzega kwamba waipandishe, basi kutokea kwanza barabara ya Kijiji kuwa ya Wilaya, halafu ndiyo hayo ya baadaye kupandishwa kuwa barabara ya Mkoa ije ifuatie baadaye. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza. Kutokana na swali la msingi (b) la Mheshimiwa Teddy L . Kasella-Bantu na kwa kuwa ahadi ni deni kwa Marais kwa ajili ya kutengeneza barabara na imejionyesha kwamba Rais wakati wa uchaguzi Mkuu alitoa ahadi ya kuhakikisha kwamba barabara ya kutoka Dodoma, Singida, Nzega mpaka Mwanza itengezewe kwa lami; Akiwa shahidi, Naibu Waziri juzi amekwama kwa siku mbili akiwa njiani kupita njia hiyo; Je, Bunge mnatuambia nini kuhusu ujenzi huo ili uharakishwe?

**SPIKA:** Hili swali kama jipya hivi, barabara kuu! Lakini, Waziri nakupa uhuru wa kuweza kujibu kwa sababu ni taarifa tu kwa nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MIUONDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MHANGA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara kuu hizi zimeahidiwa katika Ilani ya Uchaguzi. Lakini vile vile Rais alipokuwa akipita kuomba kura aliahidi kwamba barabara hizi zitajengwa na kwa kweli kama yeye anavyojua na kama Wabunge wanavyofahamu, barabara zote alizozitaja za Kati tayari wapo makandarasi, hakuna kipande ambacho hakina Mkandarasi kwa sasa.

Kwa hiyo, tatizo linaweza kuwepo tu kwamba baadhi ya Makandarasi wamecheleweshа kukamilisha miradi. Lakini, ahadi iko pale pale na barabara hizi zitajengwa katika kipindi hiki cha miaka mitano ili kutokea Dodoma hadi Mwanza tuweze kupita kwa lami kufikia kipindi hiki cha Ilani ya Uchaguzi. Ahsante sana! *(Makofi)*

Na. 4

**Barabara ya Myigo Mgololo**

**MHE MOHAMED RISHED ABDALLAH (K.n.y. MHE. BENITO W. MALANGALILA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Kiwanda cha Karatasi cha *SPM* kilichopo Mgololo hakizalishi karatasi kwa wingi hivi sasa; na kwa kuwa, sehemu kubwa ya Malighafi (magogo ya uzalishaji na umeme) inatoka Wilayani Njombe kupitia barabara ya Myigo – Mgololo; na kwa kuwa Wilaya ya Mufindi na Bodi ya Mkoa wa Iringa vimeiomba Serikali mara kwa mara kuimiliki na kuiendesha barabara hiyo:-

(a) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa umuhimu wa barabara hiyo umeongezeka sana?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa kuna umuhimu mkubwa kabisa wa kuimiliki barabara hiyo mapema iwezekanavyo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Benito William Malangalila, Mbunge wa Mufindi Kusini, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Nyigo – Mgololo yenye urefu wa kilomita 65 inamilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi. Barabara hiyo inaunganisha Kiwanda cha Karatasi cha Mgololo na Barabara Kuu ya Tanzania kwenda Zambia (*TANZAM*). Barabara hiyo ni moja kati ya barabara mbili zinazotumika kusafirisha malighafi na mahitaji mbalimbali ya wafanyakazi kwa ajili ya kuendesha Kiwanda cha Karatasi cha Mgololo. Barabara nyingine ni ile ya kutoka Mafinga hadi Mgololo ambayo ina mlima mkali *(escarpment).*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benito Malangalila, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inakubaliana na Mheshimiwa Malangalila juu ya umuhimu wa barabara hiyo na ninapenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa Wizara imeshapokea ombi la kuipandisha hadhi barabara hiyo ili iwe na Mkoa na ihudumiwe na Wizara yangu kupitia *TANROADS*. Kwa sasa Wizara inaendelea na zoezi la kutunga sheria mpya ya Barabara ambayo ndani yake barabara zote nchini na zile zilizoombewa kupandishwa madaraja ikiwemo ya Nyigo – Mgololo, zinapitiwa upya ili ziweze kupandishwa au kushushwa madaraja kulingana na vigezo vitakavyowekwa kwa mujibu wa sheria.

Kwa kuwa zoezi la kupitia sheria ya barabara lipo katika hatua za mwisho kukamilika, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Mufindi kuvuta subira hadi hapo marekebisho ya sheria hiyo ya barabara yatakapopitishwa na Bunge hili Tukufu.

**WAZIRI WA UCHUMI, MIPANGO NA UWEZESHAJI (k.n.y. WAZIRI WA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maelezo yafuatayo kuhusu *ESPM* na Mgololo hakizalishi karatasi kwa wingi hivi sasa.

Kwanza, naomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri kuhusu hii barabara ya Nyigo kwenda Njombe ambayo kwa kweli ni barabara muhimu na Serikali itakapofanya uamuzi basi italizingatia vizuri. Lakini *ESPM* haiko, iliyoko pale ni *MPM* (*Mufindi Paper Mill)* na kwamba kiwanda hiki cha *ESPM* kilibinafsishwa miaka miwili iliyopita. Wakati kinabinafsishwa kwa karibu miaka kumi kilikuwa hakizalishi chochote, sifuri. Leo kiwanda kile katika muda wa mwaka mmoja kinazalisha tani 32,000. Kwa hiyo, huwezi kusema kwamba uzalishaji hautoshi. Lazima tuwapongeze wale waliochukua kiwanda kwa sasa. *(Makofi)*

Lakini vile vile wana mipango ya kufikisha uzalishaji wa tani 350,000 mpaka tani 500,000. Kwa hiyo, juhudi zinazofanyika pale ni kubwa, sisi kama Wabunge na viongozi lazima tuwapongeze wenye kiwanda hiki kwa mipango yao hii mizuri. Lakini vile vile wanawekeza. Sasa hivi wamewekeza Dola milioni 35 za Kimarekani.

Mwaka 2006 kutokana na uzalishaji huu, wameuza tani 32,000 ambazo ni Dola milioni 18.5. Katika hizo, Dola milioni 11.5 ni *export.* Kwa hiyo, wametuongezea pato la fedha za kigeni. Kwa hiyo, mimi naomba tuwapongeze na tuwasifu kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Na. 5

**Kuhusu Mawasiliano ya Simu za Mkononi**

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA (k.n.y. MHE. KAIKA S. TELELE)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Miundombinu ya Mawasiliano hususan Simu za Mkononi ni muhimu sana katika kusukuma kasi ya maendeleo ya Wananchi wetu Vijijini pamoja na kupashana habari kwa haraka; na kwa kuwa, Wilaya ya Ngorongoro inakabiliwa na tatizo sugu la wizi wa Mifugo kutoka baadhi ya Vijiji vya Mikoa ya Mara na Shinyanga:-

(a) Je, Serikali iko tayari kuzishawishi na kuzielekeza Kampuni za Simu za mikononi kuongeza minara ya simu katika maeneo ya malisho ya mifugo (Mbuga) kama vile Kakesio, Olbalbal, Endulen, Malambo, Piyaya, Soitsambu na Ndutu ili kukabiliana na tatizo hilo kwa haraka?

(b) Je, Serikali inafahamu kuwa, kuna urasimu mkubwa wa utoaji vibali kwa kampuni hizo kuingia na kuweka minara katika eneo hilo la hifadhi ya wanyamapori na binadamu (Matumizi Mseto ya Ardhi) unaofanywa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro?

(c) Je, Serikali inasema nini kwa Shirika hilo la Umma juu ya urasimu huo unaowanyima wananchi wa Ngorongoro haki ya kasi ya maendeleo tofauti na wenzao wa maeneo mengine nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kaika Telele, Mbunge wa Ngorongoro, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja, pamoja na marekebisho yaliyofanywa kama ifuatavyo:-

Serikali inatambua umuhimu wa huduma ya mawasiliano ya simu hususan simu za mkononi katika kuharakisha maendeleo ya Taifa kiuchumi, kijamii na kiusalama, siyo tu wa mifugo bali wa raia na Taifa kwa ujumla. Ili kufanikisha azma ya kufikisha huduma za mawasiliano sehemu zote nchini zikiwemo za Kakesio, Olbalbal, Endulen, Malambo, Piyaya, Soitsambu na Ndutu, Kampuni ya *Vodacom* inatarajia kujenga mnara wa mawasiliano Endulen mara tu vibali husika vitakapopatikana kutoka Baraza la Taifa la Mazingira na mnara huo utakapokuwa tayari utahudumia maeneo ya karibu kama Endulen, Makao Makuu na hata Mbulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Kampuni ya *CELTEL*, ujenzi wa mnara wa mawasiliano katika maeneo ya Endulen na Soitsambu, utakamilika na huduma kuanza kutolewa kati ya mwezi Aprili, mwaka huu hadi Desemba, 2007. Aidha, katika maeneo mengine ya Kakesio, Olbalbal, Malambo, Piyaya na Ndutu, tathmini ya soko inatarajiwa kufanyika muda wowote kuanzia hivi sasa.

Kampuni ya *TIGO* imeweka tayari minara katika maeneo ya Endulen pamoja na Mbuga ya Wanyama ya Ngorongoro. Minara hii itasaidia na inasaidia kutoa huduma za mawasiliano katika vijiji mbalimbali Wilayani humo. Kwa kuwa ni eneo la hifadhi, siyo rahisi kuweka minara mingi katika eneo hilo kutokana na athari za kimazingira.

Tunamwomba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wavute subira wakati taratibu za uwekaji minara katika maeneo haya zinakamilishwa. *(Makofi)*

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kinachotokea katika Kijiji cha Kakesio pamoja Piyaya kule Ngorongoro ni sawa sawa kabisa, tatizo lililo katika Tarafa ya Mgoli katika Jimbo la Singida Kaskazini na Kata nzima ya Mgoli na Kata ya Ngimu hawana kabisa mawasiliano ya umeme wala simu na wanahitaji mawasiliano ya simu kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri ili na wao waendelee mbele; ninaomba kujua kama kuna mpango wowote wa haraka na wa dharura wa kuwezesha mawasiliano ya simu katika Tarafa ya Mgoli kule Singida Kaskazini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, kwamba pamoja na Tarafa zake anazozisema, pia masuala ya mawasiliano ya simu upande wa Iramba nayo pia yako katika kushughulikiwa. Siwezi kukumbuka ni Vijiji vipi, lakini Makampuni ya Simu yanayo nia ya kwenda kupeleka huduma zao za simu Mkoa wa Singida.

Napenda nichukue nafasi hii niyashukuru makampuni ya simu kwa niaba yenu Waheshimiwa Wabunge, kwamba maeneo yetu mengi yamefikiwa na tunaweza kuwasiliana. Ahsante. *(Makofi)*

Na. 6

**Swali Zima la Usimamiaji wa Mafuta**

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA** aliuliza:-

Kwa kuwa *TPDC* ndicho chombo kilichopewa mamlaka kwa Ilani ya Rais Na.140 ya mwaka 1969 ya utafutaji na uzalishaji wa mafuta na kufanya Mikataba kuwa na hisa na kadhalika; na kwa kuwa, *TPDC* iko chini ya Wizara ya Nishati na Madini na kwamba *TPDC* na Wizara ya Nishati na Madini sio vyombo vya Muungano wakati huu mafuta na gesi ni vitu vilivyoko kwenye mambo ya Muungano kwa mujibu wa Katiba ya nchi ya 1977:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa huo ni ukiukwaji wa waziwazi wa makusudi wa Katiba ya nchi kwa vyombo visivyokuwa vya Muungano kusimamia masuala ya Muungano?

(b) Kwa kuwa athari iliyokwishatokea tangu mwaka 1997 hadi leo hii kwa upande mmoja kukiuka kwa makusudi makubaliano ya Muungano ni kubwa; Je, Serikali itarekebisha vipi kasoro hiyo kwa haraka?

(c) Kwa kuwa Sheria ya uchimbaji mafuta *Act. No. 27* ya mwaka 1980 inatakiwa ifanye kazi Tanzania Bara na Zanzibar. Je, Sheria hiyo, imeridhiwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kabla hujajibu swali, napenda kukupongeza sana kwa niaba ya Bunge, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Naibu Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, napenda wakati huo huo kutambua uwepo wa mkewe Mheshimiwa Naibu Waziri Mama Blandina Ngeleja, yule pale na pia ndugu yake Bwana Novatus Kikumbizi, wametoka Jimboni Sengerema. Nadhani ni utaratibu mzuri tu, siku muhimu kama hii mtu anajibu swali lake la kwanza katika Bunge familia kuweza kuwepo. Pongezi pia kwa hilo. Sasa majibu. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, naomba niseme maneno ya utangulizi.

Mheshimiwa Spika, kwanza niungane na wewe na Waheshimiwa Wabunge wengine wote na Taifa kwa ujumla kuwapa pole familia ya Mheshimiwa Juma Akukweti na wafiwa wengine ambao wamepoteza wapendwa wetu kwa ajali ya ndege iliyotokea mwaka 2006 kule Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nitumie fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kumjalia Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kuniteua mimi kuwa msaidizi wake kwa nafasi hii ya Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, naomba pia, nitumie fursa hii kwa dhati kabisa kukushukuru sana wewe mwenyewe, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, lakini pia wapiga kura wangu ambao wameniwezesha nikaonekana na nikafika hapa kwa namna moja au nyingine kuchangia uteuzi wangu. *(Makofi)*

Lakini pia namshukuru sana mke wangu Blandina kwa sababu amekuwa msaada mkubwa sana, ameniwezesha, lakini pia amenilea kwa kipindi chote. Namshukuru sana mke wangu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Wabunge kwa kunipa moyo kwa kazi hii nzito.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno haya ya utangulizi naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni, kama ifuatavyo:-

Kabla ya kujibu swali hili, naomba kutoa ufafanuzi ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, Shirika la Maendeleo ya Petroli *TPDC* lilianzishwa kwa Sheria ya Mashirika ya Umma Na. 17 ya mwaka 1969 na Tamko la Serikali Na.140 la tarehe 30/5/1969. Madhumuni ya kuanzishwa kwa *TPDC* ni kusaidia Serikali kusimamia utafutaji na uzalishaji wa mafuta ya petroli nchini. Aidha, Sheria ya utafutaji na uzalishaji wa mafuta ya mwaka 1980 Na. 27 Kifungu Na. 16 (3) ni Sheria ya Muungano ambayo inasimamiwa na Waziri mwenye dhamana ya kusimamia Nishati wa Serikali ya Muungano. Sheria hiyo ya utafutaji na uzalishaji wa mafuta inampa Waziri mamlaka ya kuruhusu *TPDC* kufanya uchunguzi, majadiliano na kukusanya taarifa muhimu za utafutaji wa mafuta.

Hivyo, ingawa *TPDC* haikuanzishwa kama chombo cha Muungano, Sheria ya utafutaji na uzalishaji wa mafuta ambayo ni ya Muungano imekitambua chombo hicho kama sehemu muhimu katika kutekeleza sheria hiyo.

Katika kusimamia na kutekeleza Sheria ya Mafuta ya mwaka 1980, Wizara ya Nishati na Madini na *TPDC* zimekuwa zikishirikiana na Wizara inayohusika na Nishati ya Serikali ya Mapinduzi katika masuala mbalimbali yahusuyo utafutaji na uchimbaji mafuta yakiwemo kutangaza kwa wawekezaji maeneo ya utafutaji mafuta nchini, majadiliano na wawekezaji wenye nia ya kuwekeza nchini na kushiriki katika Mikutano na makongamano ndani na nje ya nchi.

Aidha, Bodi ya Wakurugenzi wa *TPDC* ina ujumbe mmoja na mafunzo ya ndani na nje ya nchi hutolewa kwa wataalam wa utafutaji, uzalishaji na usambazaji mafuta wa Serikali ya Mapinduzi, ili kujenga uwezo na kuwapatia uzoefu wataalam hao katika fani mbalimbali za Sekta ya Mafuta.

Mheshimiwa Spika, baada ya ufafanuzi huo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa shughuli za utafutaji na uzalishaji mafuta zinaongozwa na Sheria ya Muungano na kwa kuwa pande mbili zote za Muungano zinahusishwa katika utekelezaji wa sheria hiyo ni maoni ya Wizara kwamba hakuna ukiukwaji wa wazi au wa makusudi ama vinginevyo wa Katiba.

(b) Mheshimiwa Spika, suala la utafutaji mafuta Zanzibar ni moja ya kero za Muungano ambazo zinashughulikiwa na Kamati maalum ya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi, hivyo namshauri Mheshimiwa Mbunge avute subira hadi hapo Kamati itakapotoa taarifa na ushauri wake juu yasuala hilo. *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Spika, Sheria ya Utafutaji na uzalishaji Mafuta Na. 27 ya mwaka 1980 ni ya Muungano na inasimamia moja kati ya masuala 22 ya Muungano. Sheria hiyo ilijadiliwa na kupitishwa kwa mujibu wa Ibara Na. 98(1) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977 kama ambavyo imekuwa ikifanyiwa marekebisho. Aidha, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lina Wabunge wa pande mbili za Muungano na kwa mujibu wa Ibara Na. 98(1) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977 theluthi mbili ya Wajumbe toka upande wa Muungano waliridhia na sheria hiyo ikapitishwa. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mafuta na gesi ni vitu vya Muungano na kwa kuwa tangu mwaka 1977 ulipopita uamuzi huo ukaingizwa katika Katiba:-

(a) Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba madini yatakayo patikana Zanzibar na haya yaliyoko Tanzania Bara; Je, navyo ni vitu vya Muungano? *(Makofi)*

(b) Kwa upande mmoja madini yameshavunwa kwa muda muda mrefu tangu mwaka 1977 na gesi imeshavunwa tangu mwaka 2004; Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, ataniambia hisa za Zanzibar ni ngapi katika gesi na hizi za Tanzania Bara ni ngapi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba, mojawapo ya masuala ambayo Serikali za pande zote mbili zinashughulikia ni hili suala la mgao.

Kwa hiyo, bado nasisitiza kumshauri Mheshimiwa Mbunge avute subira ili tuone utaratibu bora utakavyoweza kusaidia kuboresha suala hili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Jamani Mswalie Mtume! Huyu Naibu Waziri ndio leo siku yake ya kwanza. Basi naruhusu hilo moja. *(Kicheko)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nafahamu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Vikao vya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi vimekwenda muda mrefu sana na swali hili halijapatiwa ufumbuzi; Je, haoni Mheshimiwa Waziri Mkuu umefikia wakati sasa Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kushirikishwa katika masuala haya mazito ambayo kila siku hayapati ufumbuzi? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na mimi najiunga na Waheshimiwa Wabunge kumpongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri alivyojibu maswali haya vizuri sana. *(Makofi)*

Kwa kweli majibu yangu yako pale pale. Alichosema Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba mazungumzo kati ya timu ya Waziri Mkuu na timu ya Waziri Kiongozi

yanaendelea, yanaendelea vizuri kabisa. Tunaelewana vizuri, hayajachukua muda mrefu kiasi cha kutisha wakati muafaka, Wabunge na Wawakilishi wataarifiwa juu ya matokeo ya Mikutano yetu. *(Makofi)*

Na. 7

**Madini ya Jasi – Kilwa**

**MHE. FATMA ABDALLAH MIKIDADI (k.n.y. MHE. HASNAIN G. DEWJI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Kilwa kuna hazina kubwa ya madini ya jasi ambayo yako katika Kata za Mandawa na Kilanjelanje na kwa kuwa Wilaya haipati mafanikio yoyote kutokana na madini hayo? Je, Serikali ina mpango gani na madini hayo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Wilaya ya Kilwa ina raslimali kubwa ya madini ya jasi. Kutokana na tafiti zilizofanyika mwaka 1957, zaidi ya tani milioni 3.2 zenye asilimia 92 za jasi zinapatikana maeneo ya Kata ya Mandawa na Kilanjelanje.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa, Serikali imetoa leseni za utafutaji na uchimbaji madini kwa kampuni na watu mbalimbali katika Wilaya ya Kilwa, ikiwa ni pamoja na Kata za Mandawa na Kilanjelanje alizozitaja Mheshimiwa Mbunge. Kati ya kampuni hizo, kampuni ya Kizimbani *Gypsum and Mining Prospectors* ilipata leseni mwezi Mei, 2005 na hadi kufikia Desemba, 2006 ilichimba tani 535 za madini ya jasi yenye thamani ya Sh. 11,054,475/=. Madini ya jasi huuzwa kwa kampuni za kutengeneza saruji hapa nchini na kiasi kingine husafirishwa nchi za nje kama vile Msumbiji.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ambayo Wilaya inapata kutokana na madini ya jasi ni pamoja na wananchi wa maeneo yenye madini ya jasi kuajiri katika shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini hayo na hivyo malipo wanayolipwa huinua kipato cha wananchi hao.

Aidha, fedha zinazolipwa kwa Serikali na kampuni na watu wenye leseni katika maeneo hayo kama ada za leseni na mrahaba hutumika katika mipango ya maendeleo ya nchi yetu yakiwemo maeneo ya Kata za Mandawa na Kilanjelanje. Wananchi wa maeneo hayo wanafaidika kwa kufanya biashara na kampuni hizo. Wananchi wanauza au kutoa huduma mbalimbali kwa kampuni hizo na hatimaye kupata fedha za kujiendeleza kimaisha.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango mahsusi wa kuendeleza uchimbaji wa madini hayo kwa kuhakikisha kuwa yanachimbwa kwa maendeleo ya Watanzania. Aidha, miradi ya barabara na umeme itakapokuwa imekamilika katika maeneo hayo

itachochea kwa kiasi kikubwa kasi ya uchimbaji wa madini hayo. Ili wananchi waweze kunufaika zaidi na madini hayo, Serikali inawapatia wachimbaji madini elimu ya ugani na biashara ili waweze kufaidika zaidi na madini hayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mkakati wa kuzishawishi kampuni zinazochimba madini katika maeneo hayo kutumia sehemu ya mapato yao katika kuendeleza maeneo hayo. Aidha, Serikali ina mpango wa kitaifa wa kuendeleza madini ya viwandani yakiwemo madini ya jasi. Mikakati hiyo, ni pamoja na uhamasishaji wa kampuni kuleta vifaa vya uchimbaji madini nchini, vyombo vya fedha ili vitoe mikopo kwa wachimbaji madini na uanzishwaji wa vyama vya ushirika vya wachimbaji. *(Makofi)*

**MHE. FATMA ABDALLAH MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, Je, Serikali inafahamu kwamba Mkoa wa Lindi katika Wilaya zake, Wilaya ya Kilwa, Liwale, Nachingwea, Rwanga, Lindi ina madini mbalimbali zaidi ya haya ambayo tumeyataja *gypsum?* Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia kufanya utafiti ili madini haya waweze kufaidika wananchi na Taifa? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu kwamba nchi yetu ya Tanzania imejaliwa kwa kiwango kikubwa sana kuwa na rasilimali mbalimbali. Lakini kama ilivyoelekezwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 ambayo itatupeleka mpaka 2010 mojawapo ya mambo ambayo Serikali imeelekeza hasa kupitia Sekta ya Madini ni kuendelea kufanya utafiti ili kupata takwimu sahihi za madini kama ya jasi na mengineyo ama rasilimali nyingine zinakopatikana ili tuendelee kupata manufaa zaidi kama Taifa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, naona umeanza vizuri. *(Kicheko/Makofi)*

Na. 8

**Uvuvi Haramu wa Kutumia Mabomu**

**MHE. FATMA ABDALLAH MIKIDADI** aliuliza:-

Kwa kuwa katika mwaka 1998 Serikali ilifanya *operation* maalum ya kuzuia uvuvi haramu wa kutumia mabomu katika bahari ya Hindi kwenye Mikoa ya Lindi na Mtwara kwa kutumia Meli iitwayo *"PONO", Operation* hiyo ilifanikiwa kukamata wavuvi haramu 300, mabomu kilo 185 aina ya *Ammonium Nitrate*, baruti za *Plastic Explosive EA* kilo 24, tambi za kuwashia baruti 50 na *Detonators "EA"* kilo 200 hali iliyosababisha Serikali kuahidi kupeleka *speed boat* ili kuzuia kabisa uharibifu wa mazingira kwa kufanya doria, ahadi ambayo haijatimizwa; na kwa kuwa, Tanzania imeridhia Mkataba wa kusimamia usalama wa usafiri wa majini na uchafuzi wa bahari *(The Convention of Marine Pollution by Dumping of Wastes and other matters 1972*) kwa lengo la kupata msaada wa vifaa muhimu na nyenzo za kufanyia utafiti, kudhibiti na kuzuia uchafuzi wa mazingira baharini:-

(a) Kwa kutumia Mkataba huo; Je, Serikali haiwezi kupata *speed boat* angalau moja kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara ili kuweza kudhibiti uvuvi haramu wa kutumia mabomu ambao unaharibu mazalio ya samaki?

(b) Je, Serikali inafahamu kuwa samaki wanaovuliwa kwa mabomu ni sumu kwa binadamu na ina mpango gani wa kuzuia tatizo hilo ili kuwanusuru wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Sheria ya uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 na Kanuni za Uvuvi za mwaka 2005 imepiga marufuku uvuvi haramu ukiwemo wa kutumia vifaa vya milipuko kwa mfano baruti. Idara ya uvuvi ina kitengo cha doria na udhibiti ambacho kinasimamia shughuli za kudhibiti uvuvi haramu nchini.

Katika mwaka wa fedha wa 2006/2007 Wizara ya Maliasili na Utalii, imenunua maboti matatu yaendayo kwa kasi kwa ajili ya kusambazwa kwenye vituo vya doria.

Aidha, boti moja yenye urefu wa mita 12 itapelekwa kwa ajili ya doria katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Kwenye mwaka wa fedha wa 2007/2008 Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa kupitia Idara ya Uvuvi, imepanga kuanzisha rasmi kituo cha doria kwa ajili ya Mikoa hiyo ya Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, suala la udhibiti uvuvi haramu wa kutumia mabomu haliwezi kudhibitiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii peke yake. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara na Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Usalama wa Raia, Miundombinu na Nishati na Madini kwa pamoja tumefanya tathmini ya ukubwa wa tatizo, athari zake na jinsi ya kulikabili. Mapendekezo yatawasilishwa kwenye ngazi za juu Serikalini kwa hatua za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa samaki waliovuliwa kwa kutumia mabomu wanaweza kuwa na madhara. Vile vile uvuvi wa kutumia mabomu huharibu mazalio ya samaki, viumbe hai pamoja kujeruhi au kukua wavuvi wanayoyatumia.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatoa wito kwa Halmashauri kushirikiana na wananchi wote pamoja na vikundi vya ulinzi wa rasilimia *(beach management units)* kulinda rasilimali katika maeneo yao na kusaidia juhudi za Serikali za kukomesha uvuvi haramu kwa manufaa ya wananchi, Taifa letu na kizazi kijacho.

**MHE. FATMA ABDALLAH MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini napenda kufahamu kwa kuwa

hawa wavuvi haramu 300 ambao wanajulikana kwa majina, kwa Mtaa wanaoishi na Kijiji wanachoishi, tunawasaidiaje kwa sababu hawa ni mabingwa wa kupiga mabomu, wajuzi wa kupiga mabomu, wajuzi wa kuvulia nyavu za aina zote. Sasa je, Serikali haiwezi kuwasajili ikaweza kuwakopesha angalau kwa awamu kwa kila mwaka ili wawe na nyavu halali mbadala badala ya mabomu? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kitu cha msingi kabisa kinachotakiwa kufanywa kwa hao wavuvi ambao wamebobea katika uvuvi haramu kwanza ni kupata elimu waweze kufahamu kwamba uvuvi haramu wa kutumia mabomu wa kutumia nyavu zenye macho madogo sio uvuvi endelevu. Lakini, pili, tuna mradi wa *MANTEP* ambao huwa unasaidia vikundi vinavyohusika na masuala ya uvuvi. Hivyo kwa basi kwa kuwa unawafahamu Mheshimiwa Mbunge, wajiunge wafanye kikundi ili waweze kupata msaada wa kununua vifaa vya kuvulia ambavyo ndiyo vifaa vinavyoleta uvuvi endelevu watapata msaada kutoka mradi wa *MANTEP*. *(Makofi)*

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. Vile vile napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Mheshimiwa Naibu Waziri, alipokuwa anajibu swali la msingi alikuwa amekemea sana suala la baruti na mimi naipongeza sana Serikali kwa suala hilo. Lakini je, Serikali inasemaje kwa wale wavuvi ambao wamefanya mbadala wa uvuvi na kutumia bunduki ambazo haziharibu mazingira, hazina baruti, lakini pia wavuvi hao huwa wanachukua samaki wa aina fulani katika kupiga samaki hao ili wapate manufaa na kujiendeleza maisha yao?

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kutufahamisha kwamba kuna wavuvi ambao wanavua kwa kutumia bunduki. Kusema kweli uvuvi huu ni uvuvi haramu na hautakiwi kufanyika kwa sababu unaharibu mazingira na si uvuvi endelevu. Nitamwomba Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, aweze kutueleza ni maeneo gani ambayo wanavua kwa kutumia bunduki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nadhani tuendelee Waheshimiwa Wabunge. Wizara hiyo hiyo ya Maliasili na Utalii swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, Tabora.

Na. 9

**Chuo cha Nyuki - Arusha**

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mkoa wa Tabora umezungukwa na miti ya Miombo *(Miombo Wood Land)* ambayo ni mahsusi kwa kutoa maua yanayotumiwa na nyuki kutengeneza asali; na kwa kuwa, Chuo cha Nyuki kilichokuwa Mkoani humo kilihamishiwa Olmotonyi, Arusha ambako hakuna miti ya aina hiyo; na kwa kuwa, chuo hicho tangu kilipoanzishwa

Tabora mwaka 1974 kilifundisha hata wageni toka nje ya nchi waliokuwa wanajionea hali halisi ya jinsi asali inavyotengenezwa:-

Je, kulikuwa na sababu zipi zilizosababisha Serikali ikihamishe chuo hicho na kukipeleka Arusha?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mbunge Viti Maalum kuwa Serikali ilihamisha Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki kutoka Tabora kwenda Chuo cha Misitu cha Olmotonyi, Arusha mwezi Julai, 1995. Uamuzi huo ulichukuliwa kwa sababu wanafunzi waliokuwa wanaomba kujiunga na Chuo hicho walikuwa wachache. Hali hiyo iliathiri pia wanafunzi toka nchi za nje ambao kimsingi kama wangeendelea kusoma Tabora, gharama za uendeshaji zingekuwa kubwa. Kwa wakati huo ilionekana kuwa kwa kuunganisha vyuo hivyo viwili, Serikali ingeweza kubana matumizi katika maeneo yafuatayo:-

(i) Matumizi ya vifaa vya kufundishia vya darasani na maabara;

(ii) Kuwatumia walimu wachache katika masomo yanayofanana;

(iii) Matumizi ya vifaa vya kufundishia mafunzo kwa vitendo kwa mfano magari;

(iv) Gharama za uendeshaji kwa mfano simu, umeme na maji yangepungua kwa kuwa na Chuo kimoja; na

(v) Vile vile *supporting staff* wangetumika wachache kwa kuwa na Chuo kimoja.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekwishaamua kuipa Sekta ya Ufugaji Nyuki kipaumbele katika kuimarisha utafiti, mafunzo na shughuli za ugani ili kuipa uwezo sekta hii wa kuchangia kikamilifu katika kukuza uchumi, kuondoa umaskini na kuboresha hifadhi ya mazingira. Kwa hiyo, Wizara yangu imeamua kurudisha mafunzo ya ufugaji nyuki Tabora na kukifufua Chuo hicho haraka iwezekanavyo ili Taifa liweze kupata wataalamu wa kutosha katika fani ya nyuki.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaandaa mipango na taratibu za kukirudisha Chuo cha Nyuki, Tabora.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya kuridhisha ya Serikali nina swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo: -

Je, ni lini sasa mkakati huo utaandaliwa na lini chuo hicho kitaanza ili kuweka rekodi sawa katika *Hansard* kwa kumbukumbu zote za baadaye kwamba ni lini Serikali inatarajia kukianzisha Chuo hicho. Ahsante Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi kwamba Wizara inaandaa mipango na utaratibu wa kukirudisha Chuo cha Nyuki, Tabora. Katika mwaka huu wa fedha tunaanza matayarisho lakini katika mwaka 2007/2008 Chuo hicho kitaanza masomo huko Tabora. *(Makofi)*

Na. 10

**Utoaji Mimba**

**MHE. HAROUB SAID MASOUD** aliuliza:-

Kwa kuwa utoaji mimba umekithiri sana hapa nchini; na kwa kuwa watu wengi wanaotoa mimba ni watoto wa shule.

(a) Je, ni wakati gani wanawake wanaweza kuruhusiwa kutoa mimba?

(b) Je, ni madaktari wenye sifa gani wanaoruhusiwa kuidhinisha utoaji wa mimba kwa dharura maalum?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mbunge wa Koani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kulingana na sheria ya nchi yetu utoaji wa mimba ni kuvunja sheria isipokuwa pale ambapo ushauri wa Daktari kama sehemu ya tiba, bali mimba inaweza ikaruhusiwa ikatolewa. Sababu hizo ndizo ambazo zinaashiria kuhatarisha maisha ya mama endapo mimba itaendelea kukua.

(b) Madaktari wanaoruhusiwa kuidhinisha utoaji wa mimba kwa sababu maalum ni jopo la madaktari bingwa wa magonjwa ya akinamama watatu akimhusisha daktari bingwa mmoja wa ugonjwa unaosababisha ile mimba kutolewa; kwa mfano Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Moyo anaweza kuhusishwa kama hali ya mgonjwa wake wa moyo ikizidi kuwa mbaya kama ataendelea kuwa mjamzito.

**SPIKA:** Bado jibu halijakamilika.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, samahani. Serikali imeweka jitihada za makusudi za kuelimisha jamii kuhusu athari za utoaji wa mimba katika mazingira ambayo siyo ya kitalaamu kwa lengo la

kupunguza vifo vinavyotokana na utoaji wa mimba. Hii ni pamoja na kutoa ushauri kwa wale wanaopata matatizo ya mimba kutoka ili kuweza kuzuia tatizo hilo lisitokee tena. Aidha, ushauri husika ni pamoja na matumizi ya dawa za uzazi wa mpango, matibabu ya magonjwa mfano yanayotokana na kujamiiana.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa juhudi za Serikali na za wanaharakati zilisaidia sana kupunguza tatizo la ukeketaji hapa nchini, sasa je, Serikali haioni kwamba sasa ni muda muafaka kutumia juhudi kama hizo ili kuwazuia wale baadhi ya vibibi vizee ambavyo wanatoa mimba ya watoto wadogo kwa kutumia mizizi ya miti aina ya mihina? *(Kicheko)*

**SPIKA:** Sikusikia vizuri, sijui Naibu Waziri amesikia, mizizi?

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja nyongeza.

Kwa kuwa juhudi za Serikali na wanaharakati hapa nchini zilisaidia sana kupunguza tatizo la ukeketaji nchini, je, Serikali haioni kwamba sasa ni muda muafaka wa kutumia juhudi hizo hizo ili angalau kupunguza matatizo ya utoaji wa mimba ambao baadhi ya vibibi vizee hutumia utoaji wa mimba hiyo kwa kutumia mizizi aina ya mihina? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kutoa mimba wale ambao wanatoa mimba wanatumia njia nyingi ikiwemo hiyo aliyoitaja Mheshimiwa Haroub Said Masoud ya kutumia mizizi ya mihina. Ninachotaka kuzungumza hapa ni kwamba kutoa mimba iwe unatumia mizizi au unatumia vifaa vyovyote vile kutoa mimba ni kosa la jinai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naomba niseme kwamba kama mtu atapatikana anatoa mimba awe ametumia njia yoyote ile iwayo, basi anabidi achukuliwe hatua. Serikali yangu bado inaendelea kutoa wito kwamba mimba zinazuilika. Haiwezekani mtu akasema amepata mimba kwa bahati mbaya kwa sababu ya uzazi wa mpango upo. Lakini vile vile kupata mimba siyo tu kunahatarisha maisha yako lakini vile vile unaweza kupata matatizo ya ugonjwa wa UKIMWI na maambukizi mengine kwa sababu unapopata mimba umetumia njia ambazo siyo za kuzuia kupata matatizo mengine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla tujue kwamba kutoa mimba ni kosa na wale vibibi vizee na wale vijana na madaktari wengine wote na wale wataalam wa afya ambao wanatoa mimba kwa wananchi waache mara moja kwa sababu hilo ni kosa la jinai. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Nimshukuru pia Naibu Waziri kwa majibu yake.

Mheshimiwa Spika, lakini ningependa anihakikishie kwa kuwa jibu lake limejielekeza kuokoa maisha ya mwanamke, je, ni haki kutoa maisha ya yule mtoto au ni haki kuokoa maisha ya wote wawili kadri inavyowezekana?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, mama anapokuja akiwa mjamzito nafahamu katika haki za binadamu si vizuri kutoa mimba kwa sababu kile kiumbe kilichokuwa tumboni kinastahili kuishi.

Mheshimiwa Spika, kitaalam yule mtoto bado hatujamwona, lakini mama hapa tunamwona naye tunajua kuwa anaishi. Hatuwezi kujua baadaye kama yule mtoto atakuwa ni mtoto au itakuwa ni nini. Kinachozungumziwa hapa ni afya ya yule mama ambaye kwa sasa hivi yuko hapa.

Mheshimiwa Spika, naamini kabisa kwamba kuliko kuacha mama apoteze uhai wake tunaamini kwamba kutoa ile mimba ili aweze kuendelea kuishi tuweze tukampa msaada zaidi na kuweza kushi na tukamshauri jinsi gani na wakati gani aweze kutoa mimba na hatimaye kwa uangalizi zaidi anaweza akapata mtoto mwingine.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba inapotokea kwamba mama anaambiwa kwamba atoe ile mimba jopo limekaa, wataalam wameona na wakaona kwamba ni bora kuokoa maisha ya mama kuliko kumwacha aendelee tutakuwa tumepoteza mtoto na tutapoteza na mama. *(Makofi)*

Na. 11

**Uanzishwaji wa Hospitali ya Apollo Hapa Nchini**

**MHE. DR. ALI TARAB ALI (k.n.y. MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI)** aliuliza:-

Kwa kuwa inafahamika kwamba Serikali kupitia Wizara ya Afya Tanzania na Hospitali ya Apollo iliyopo nchini India, waliingia katika mazungumzo juu ya makubaliano ya kutaka kuanzisha Hospitali ya Apollo hapa Tanzania zaidi ya miaka miwili iliyopita.

Je, utekelezaji wa jambo hilo umefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Hospitali ya Apollo nchini India hawajawahi kufanya mazungumzo yoyote juu ya makubaliano ya kutaka kuanzisha Hospitali ya Apollo hapa nchini. Mazungumzo ambayo

yamekuwa yanafanyika yalikuwa kati ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* na *Apollo Group of Hospitals*. Hatimaye pande hizo mbili zilisaini mkataba *(memorandum of understanding)* tarehe 6 Aprili, 2006 ambapo Balozi wetu nchini India alishuhudia.

Mheshimiwa Spika, inatarajiwa kuwa ujenzi huu utatekelezwa baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu na kuona kama mradi huu utakuwa wa faida/mafanikio kibiashara. Shirika limepokea taarifa ya makisio kutoka *Apollo Group* kwamba mradi huu unatarajiwa kugharimu kiasi cha dola za Marekani 50 milioni. Fedha hizi zitagharimiwa kwa pamoja kati ya *NSSF* na *Apollo Group of Hospitals*.

Mheshimiwa Spika, makubaliano yaliyofanyika ni kwamba Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* litatafuta kiwanja na kujenga majengo yote yanahitajika na *Apollo Group of Hospitals* wataleta vifaa husika *(Machinery and Equipment)* pamoja na wataalam mabingwa katika nyanja mbalimbali ili kuendesha hospitali hiyo. Aidha, kutakuwa na utaratibu wa kuwapatia Watanzania taaluma muhimu ili baadaye nafasi nyingi zichukuliwe na Watanzania wenye sifa husika.

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri je, hatuoni kwamba ni faida kwetu sisi tukaharakisha mazungumzo haya ili tupunguze wagonjwa wanaokwenda nje kutibiwa waweze kutibiwa hapa hapa nyumbani?

Na vile vile madaktari wetu watapata taaluma zaidi na patakuwa na *transfer of technology?*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi. Mazungumzo yamefanywa kati ya *NSSF* na *Apollo Group of Hospitals* na wenyewe wameshazungumza na wakaandikiana *memorandum of understanding*. Sasa hivi kama nilivyosema kwamba wanatafuta kiwanja na kuweza kufanya michoro na kukubaliana.

Sisi kama Serikali, sisi hatuna masuala ya kuharakisha haya mazungumzo. Kwa sababu mazungumzo yamekwishaazungumzwa. Cha msingi hapa labda ni kushauri kwamba *NSSF* na *Apollo Hospitals* waendelee sasa na ile mipango/mikakati ili waweze kuijenga hiyo hospitali. Lakini sisi kama Serikali hatuna haja kwamba tushughulikie hayo mazungumzo kwa sababu mazungumzo yameshasemwa na *memorandum of understanding* iko tayari.

Na. 12

**Gari - Gereza la Biharamulo**

**MHE. PHARES K. KABUYE** aliuliza:-

Kwa kuwa wafungwa wa Gereza la Wilaya ya Biharamulo hukata kuni katika mji huo kwa ajili ya kuni na kubeba kuni hizo kichwani:-

Je, ni lini Serikali italipatia Gereza hilo gari ili liwasaidie katika kubeba kuni pamoja na kazi nyingine gerezani hapo au kuwapatia umeme ili kunusuru mji wa Biharamulo usigeuke jangwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Phares Kabuye, Mbunge wa Biharamulo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Gereza Biharamulo linalo gari lenye namba *STJ 2327, Kia Ceres Pickup* ambalo ni zima, ingawa sasa hivi limekuwa la zamani. Gari hilo lilikuwa na tatizo la matairi na breki. Kwa sasa gari hilo limetengenezwa na linafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni kuyapatia magereza yote nchini magari kwa ajili ya usafiri na usafirishaji. Hata hivyo kutokana na ufinyu wa bajeti, Serikali itaendelea kutekeleza jukumu hili kwa kununua magari kwa awamu na kuyagawa katika magereza mbalimbali kwa kuzingatia vigezo kama vile umbali uliopo kati ya gereza na huduma za kijamii zilizopo, wingi wa wahalifu walioko gerezani na kiwango cha huduma ya uchukuzi inayohitajika katika kituo hicho. Katika mwaka wa fedha 2004/2005, Serikali imeupatia Mkoa wa Kagera lori la tani saba aina ya Isuzu yenye namba za usajili *STK 1096* kwa ajili ya uchukuzi wa mizigo pamoja na kusomba kuni kwenye vituo vyote vya mkoa, likiwemo gereza la Biharamulo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka utaratibu wa kununua magari kwa ajili ya matumizi ya Magereza ya Wilaya kila mwaka kutokana na fedha zinazopatikana na kuyagawa kwa kufuata vigezo nilivyovitaja hapo juu.

Mheshimiwa Spika, ili kuondokana na tatizo la uharibifu wa mazingira unaosababishwa na kukata miti kwa ajili ya kuni za kupikia chakula cha wafungwa na mahabusu magerezani, Jeshi la Magereza linafanya utafiti wa kutumia nishati mbadala. Utafiti huo unalenga katika kubainisha tofauti ya gharama za umeme, makaa ya mawe na gesi katika matumizi ya kupikia chakula cha wafungwa. Aidha, juhudi za kupanda miti kwa ajili ya kuni, matunda na uhifadhi wa mazingira zinafanywa katika magereza mbalimbali nchini.

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Nakushukuru sana, swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mkoa wa Kagera una Wilaya nane. Mheshimiwa Waziri anafikiri kwamba lori moja linaweza likatimiza matakwa ya wafungwa kwa Wilaya nane? *(Makofi)*

Pili, kwa kuwa *TANESCO* Biharamulo imejaribu kuweka umeme katika gereza la Biharamulo lakini wanakosa vifaa vya kupikia vya kutumia umeme. Mheshimiwa Waziri anaweza akakubali kwamba gereza la Biharamulo atalipatia vifaa vinavyoweza vikapika kwa kutumia umeme?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge, kwamba Mkoa wa Kagera ni mkubwa na ndiyo maana tumemweleza kwamba Gereza la Biharamulo linalo gari pamoja na kwamba ni gari zee. Pale ambapo gari lile ambalo tumelipatia Mkoa linaweza likafika Biharamulo litaendelea kufanya kazi na pale ambapo Serikali itapata fedha za kuweza kupeleka gari lingine katika Gereza la Biharamulo gari litapelekwa.

Kuhusu suala la kununua vifaa vya kupikia vya kutumia umeme katika gereza la Biharamulo, nilivyoeleza katika jibu langu la msingi Wizara yangu inafanya kazi sasa hivi kuangalia tofauti ya bei na gharama ya kutumia aina ya nishati mbadala katika magereza yetu mbalimbali hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika wiki mbili zilizopita Mheshimiwa Waziri amesafiri nje ya nchi kuelekea Rwanda kuangalia uwezekano wa kutumia *biogas* katika magereza yetu na mimi mwenyewe katika wiki iliyopita nimekuwa na mkutano na *TPDC* pamoja na *Pan African Energy* kuangalia uwezekano wa kutumia *compress natural gas* katika baadhi ya magereza yetu hapa nchini.

Ningeomba kwamba Mheshimiwa Mbunge, avute subira Wizara yetu iendelee kuangalia gharama tofauti mbalimbali katika kutumia nishati mbadala ili tuweze tukapanga ni aina gani ya nishati tutatumia katika magereza yetu mbalimbali hapa nchini. *(Makofi)*

Na. 13

**Kisiwa cha Mayote Kutawaliwa na Ufaransa**

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa Kisiwa cha Mayote kilichoko Comoro bado kinatawaliwa na Ufaransa, je, Umoja wa Afrika *(AU)* inafanya juhudi gani kuhakikisha kuwa Ufaransa inaiachia Comoro Kisiwa chake?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA (MHE. DR. CYRIL A. CHAMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kisiwa cha Mayote, sambamba na visiwa vingine vitatu vya Ngazija, Anzuani na Mwali vilivyomo katika Muungano wa visiwa vya Comoro, viliwekwa chini ya himaya ya Ufaransa mwaka 1843. Mwaka 1974 wananchi walipiga kura ya maoni ili kuamua endapo wangebakia chini ya umiliki wa Ufaransa au wangekuwa huru. Katika kura ile visiwa vitatu vya Comoro vya Ngazija, Anzuani na Mwali viliamua kwa asilimia 96 kuwa huru kutoka utawala wa Kifaransa. Kisiwa cha

nne cha Mayote kiliamua kwa asilimia 63.8 kubaki chini ya utawala wa Ufaransa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, kura nyingine ya maoni iliyopigwa mwaka 1975 katika kisiwa cha Mayote pekee iliamua kwa asilimia 99.4 kuwa kisiwa hicho kiendelee kuwa chini ya utawala wa Ufaransa.

Mhesahimiwa Spika, Umoja wa Afrika ungependa kuona Mayote inarudi katika dola ya Comoro, lakini changamoto zilizopo katika kufanikisha azma hii ni tatu:-

(1) Ufaransa ambayo inapendelea kukitawala kisiwa hicho ni Taifa lenye kura ya turufu katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa na hivyo inaweza kupinga pendekezo lolote linalokusudia kukiweka kisiwa hicho chini ya utawala wa Comoro.

(2) Kama nilivyoeleza hapo juu raia wa Mayote wenyewe wamepiga kura mara mbili na kuamua kubaki chini ya mamlaka ya Ufaransa.

(3) Viongozi wa ndani wa kisiwa cha Mayote wanapendelea zaidi kuwa chini ya Ufaransa kuliko kujiunga na wenzao wa Muungano wa Comoro.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hizo, Umoja wa Afrika hauna nguvu ya kuingilia maamuzi ya raia wa Mayote na kuwaondoa Wafaranasa wakati wananchi wa Mayote wenyewe wameridhia kuwa chini ya Taifa hilo kubwa.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali la nyongeza. Kutokana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, anataka kuliambia Bunge hili kwamba sasa Umoja wa Afrika hauna kauli juu ya ukoloni unaoendelea katika nchi hiyo ya Comoro?

La pili, je, ni haki Wafaransa kuendelea kutamani kutawala Kisiwa cha Comoro wakati dunia nzima watu wanataka wajitawale wenyewe?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA (MHE. DR. CYRIL A. CHAMI):** Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba Bara la Afrika, Umoja wa Afrika hauna kauli kuhusu ukoloni unaoendelea. Jambo nililosema ni kwamba Bara litachukua hatua na kuisemea sehemu yoyote ya Bara la Afrika kama sehemu yenyewe inapenda kujiondoa katika ukoloni. Ukiangalia hata historia katika nchi zote za Afrika wale ambao wamesaidiwa na wale ambao wameonyesha kwa dhati kabisa kwamba wanapenda kujiondoa katika ukoloni. Sasa hawa wenzetu wamepiga kura wakaona kwamba wangependa kubaki katika himaya ya Ufaransa na hatuwezi sisi kwenda kuingilia kule kupeleka majeshi kwa ajili ya kuiondoa Ufaransa.

Pili, suala la kwamba ni haki, Umoja wa Afrika ungependa zaidi kuheshimu kauli ya wananchi wale wa Mayote. Wao ndiyo wanajua zaidi kwamba ni haki ama siyo haki na sisi tutaendelea kuiheshimu hiyo haki yao au huo utashi walionao wao. *(Makofi)*

Na. 14

**Upimaji wa Mashamba Vijijini**

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ina mipango kabambe ya kuinua kilimo nchini kwa kutenga shilingi trilioni 2.6 kwa kipindi cha miaka saba chini ya mpango wa *ASDP* kwa wananchi wa vijijini; na kwa kuwa mpango mzuri na endelevu ni ule unaofanywa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kupitia mipango Miji kwa kutenga maeneo ya makazi na viwanja katika madaraja mbalimbali *(Low, Medium* na *High density)* pamoja na viwanja kwa ajili ya viwanda; na kwa kuwa wanavijiji wengi wanalima kiholela bila ya mashamba yao kupimwa kitaalam na hivyo kukosa miundombinu mbalimbali ya kurahisisha kilimo:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuanzisha utaratibu wa kuyapima mashamba hayo na yapangwe kitaalam?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kwa kupima mashamba hayo kwa mpango maalum itasaidia kusimamia uzalishaji wa kila mwanakijiji kitaalam katika kufikia malengo ya uzalishaji?

(c) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa pesa zinazotengwa kwa ajili ya mpango wa *ASDP* zitakuwa zinatumika vizuri katika mpango mzima wa kilimo vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, lenye sehemu (a), (b) na (c) naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, inasimamia matumizi ya ardhi mijini na vijijini kwa mujibu wa sera, sheria, kanuni na taratibu zilizopo. Upangaji wa matumizi ya ardhi vijijini unasimamiwa na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999. Sheria hii pamoja na kanuni zake, inaelezea utaratibu wa kupima na kumilikisha ardhi vijijini.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kumilikisha ardhi wananchi ili kuwawezesha kutumia ardhi kama mtaji wa kujiendeleza. Wizara yangu inaendelea kupima mipaka ya vijiji ili kwanza ardhi yote ya kijiji itambuliwe na kupewa cheti na pili kupima mashamba ndani ya kijiji na kutoa hatimiliki za kimila. Hadi sasa

vijiji vipatavyo 6,500 kati ya vijiji 14,000 nchi nzima vimepimwa. Mwaka huu wa fedha Wizara inatarajia kupima vijiji 3,104 nchini kote.

(b) Mheshimiwa Spika, usimamizi wa kilimo ni jukumu la Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Hivyo, mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa kila kijiji unaiwezesha Wizara hiyo kuwa na utaratibu wa kusimamia mpango wake wa *ASDP* vizuri kwani maeneo ya kilimo na mashamba huweza kufahamika bayana baada ya Wizara yangu kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi.

(c) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inatambua na kuthamini mpango wa *ASDP* ambao unasimamiwa na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika hivyo, kwa kushirikiana na Wizara hiyo inahakikisha wananchi wote wana ardhi kwa ajili ya kilimo na matumizi mengine. Upimaji wa vijiji na uandaaji wa mpango bora ya matumizi ya ardhi unaofanywa na Wizara yangu na ni mchango tosha kwa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika hii ni katika kutekeleza mpango wa *ASDP*. Aidha, kutenga maeneo ya kilimo kunatoa fursa kwa mpango wa *ASDP* kutekelezwa kwa ufanisi kulingana na misingi ya kilimo bora. Hivyo napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako Tukufu kuwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inafanya juhudi kuhakikisha kuwa sekta zote zinazohitaji ardhi kwa ajili ya maendeleo hazikwami.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, atakubaliana na mimi kwamba iko Mikoa yenye mipango endelevu kwa maana ya kupanga mashamba ya wanavijiji na hatimaye kuwa na miundombinu mizuri wameweza kufanikiwa katika kufanikisha suala zima la kilimo na hivi sasa wamepiga hatua.

Je, yale maeneo ambayo hayana mpango kama huo kwa mfano ule mpango ulioko katika Mikoa ya Kilimanjaro na Mbeya, haioni kwamba kuna umuhimu sasa kutoa miongozo wa mipango kama hiyo kwa makusudi ili wananchi hawa wafanikiwe katika kilimo chao?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kufuatana na sheria Na. 5 ya Ardhi ni kwamba ni wajibu wa Serikali kupanga matumizi ya ardhi kwa kazi zote na namhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba utaratibu wa mwaka huu tumekwishaanza kupanga matumizi bora ya ardhi katika maeneo kadhaa kwa mfano maeneo ambayo tutahamishia mifugo, maeneo ya kilimo na tunaendelea kwa kipindi cha mwaka huu na mwaka ujao kuhakikisha kwamba mpango huo umekamilika ili kuweza kusaidia wananchi kulima kwa ufasaha na kuweza kuendeleza kilimo katika maeneo yao.

**SPIKA:** Maswali yamekwisha na muda wa maswali pia umekwisha. Kabla sijamwita Katibu kwa hatua inayofuata ambayo ni Kusomwa kwa Mara ya Kwanza kwa Miswada ya Sheria ya Serikali, ningependa kusema kwamba Muswada wa tatu, *The Law School of Tanzania Bill* na Muswada wa tisa, *The Prevention and Combating of*

*Corruption Bill, 2007* hii itasomwa Mara ya Kwanza tarehe 8 Februari, 2007 ili kukidhi matakwa ya sheria inayohitajika kwamba Miswada hii ambayo ilichapishwa tarehe 19 iweze kuiva kwa zile wiki tatu. Katibu kwa Miswada iliyosalia.

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**Muswada wa Sheria ya Usajili wa Biashara wa Mwaka 2006 *(The Business Activities Registration Bill, 2006)***

**Muswada wa Sheria ya Kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2006 *(The Written Laws (Misc. Amendment) (No.2) Bill, 2006)***

**Muswada wa Sheria kwa Ajili ya Kuweka Mwongozo wa Kuandaa, Kuendesha na Kutekeleza Sheria ya Mipango ya Ardhi na Mambo yanayohusiana nayo *(The Land Use Planning Bill, 2006)***

**Muswada wa Sheria kwa Ajili ya Kuanzisha Bodi ya Usajili ya Mipango Miji, Udhibiti wa Viwango, Vitengo na Shughuli za Mipango Miji na Mambo yanayohusiana nayo *(The Town Planners (Registration) Bill, 2006)***

**Muswada wa Sheria ya kuweka Mwongozo wa kuandaa na kutekeleza sheria ya mipango miji kukabiriana na masuala mbalimbali yanayohusu Mipango Miji pamoja na Mambo Mengine yanayohusiana nayo *(The Urban Planning Bill, 2006)***

**Muswada wa Sheria kwa Ajili ya Kuweka Misingi na Taratibu za Mishahara, Posho, Marupurupu na Maslahi mengine ya Majaji wa Mwaka 2006 *(The Judges (Remuneration and Terminal Benefits Bill, 2006)***

**Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Kusimamia Uvuvi kwenye Bahari wa Mwaka 2006 *(The Deep Sea Fishing Authority (Amendment) Bill, 2006)***

*(Miswada iliyotajwa hapo juu ilisomwa Bungeni kwa mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa shughuli zilizopangwa kwa leo kama nitakavyoeleza hapo baada ya matangazo, kwa hiyo, natoa matangazo kwanza.

Tunao wageni katika ukumbi upande wa mkono wangu wa kulia ni vijana wa *TAYOA* kutoka Dar es Salaam wamekuja kujifunza na kuona jinsi shughuli za Bunge

zinavyoendeshwa, karibuni vijana nawaomba msimame ili Wabunge waweze kuwaona, ni wale pale. *(Makofi)*

Karibuni sana na nina imani miongoni mwenu wamo ambao watakuja kuingia katika ukumbi huu kwa njia sio ya ugeni ila kwa kuwa ni Wabunge kamili, tunawatakia heri katika maisha yenu.

Mheshimiwa Eustace Katagira, kwanza pole kwa msiba uliokukuta, anatoa taarifa ya mgeni ndugu yake Bwana Valentini Kamugisha ambaye ni mhamasishaji mkubwa wa vijana na mpiga kampeni mkubwa katika Jimbo la Kyerwa amekuja naye kujionea matunda ya kazi aliyoifanya mwaka juzi na hakika anaonyesha ni mtu matata kweli kweli.

Vikao, Mheshimiwa George Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala anawatangazia Wajumbe kwamba leo saa saba mchana ukumbi Na. 219 kutakuwa na mkutano wa kujadili Miswada ya Sheria, Wabunge wote ambao n wajumbe wa Kamati hii ya Katiba, Sheria na Utawala wanaombwa kuhudhuria saa saba mchana ukumbi Na. 219 jengo la utawala leo.

Mheshimiwa John Cheyo, anaomba kwamba leo, saa tano asubuhi. Haitawezekana kwa sababu tuna semina, nadhani hii itakuwa saa saba mchana chumba Na. 231 jengo la utawala gorofa ya pili kutakuwa na Kikao cha Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC).*

Waheshimiwa Wabunge, kumetokea misiba kwa wenzetu kama ifuatavyo, Mheshimiwa Eustace Katagira, alifiwa na mama yake mzazi tarehe 6 Desemba, 2006 Bukoba na Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, alifiwa na baba yake mzazi tarehe 17 Novemba, 2006 huko Iringa wakati wa Mkutano wa Tano wa Bunge, Mheshimiwa Eliata Nandumpe Switi, Mbunge wa Viti Maalum Rukwa amefiwa na mama yake mzazi jana wakati wa Mkutano huu wa Sita. Taratibu za ofisi zinaendelea ili kama kawaida utaratibu wetu wa kuwafariji wenzetu kwa ubani uweze kukamilishwa kwa kila mtu kwa stahili yake.

Waheshimiwa Wabunge, nimeendelea kupokea malalamiko kwamba baadhi yetu wanakerwa sana na mashindano ya kulinganisha Wabunge kwa Wabunge, Mawaziri kwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Naibu Mawaziri na kadhalika na waliniomba labda nitoe tamko la kukemea magazeti yanayohusika, nimeamua kwamba hii si sahihi kutoa tamko lolote kwa kweli kwa sababu mtu yeyote makini anajua kwamba uongozi haupimwi kama mashindano ya urembo.

Kwa hiyo, mimi nadhani la msingi kila mmoja wetu pale alipo kama ni jimbo kama ni Naibu Waziri kama ni Mkuu wa Mkoa, kama ni Waziri kamili atimize wajibu wake kwa nchi yetu kwa uaminifu na wapiga kura wataelewa, lakini haya mashindano ya kusema nani anamzidi nani wakati watu wanafanya kazi tofauti kabisa huwezi kulinganisha Wizara kwa Wizara kwa mfano mimi nayaona hayo ni namna tu ndio uhuru

ambao tumevipa vyombo vya habari. Kwa hiyo, tuwaachie mimi nadhani tupuuze tu badala ya kuingia katika malumbano na vyombo vya habari. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge baada ya matangazo haya nitaahirisha kikao chetu cha leo ili tuhudhurie semina muhimu sana, semina inayohusu mambo yetu ya ulinzi na usalama katika nchi. Kwa hiyo, saa tano kamili semina itaanza katika ukumbi wa Pius Msekwa na nadhani tutamalizia kufikia saa sita na nusu, saa saba wataalamu wakiongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa Usalama wa Taifa, wako tayari na ni somo muhimu sana kwetu sote kuelewa kwa upana jinsi usalama wa viongozi na nchi ulivyo na sio tu kwa nchi na jinsi unavyohusiana na dunia nzima.

Lingine ni kwamba kuna Miswada ambayo tunahitaji kuipitisha kwa hatua zote katika mkutano huu, sasa nimeona ni vema tutumie nafasi ya mchana leo, Kamati husika zifanyie kazi Miswada hiyo, ili kwa ile miwili iliyokwishaiva ikianza tusiwe tunawahangaisha tena

Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati kuwa wanatoka bila kuchangia ile Miswada mingine miwili. Kwa sababu hiyo nimeona ni vema basi Kamati husika na wamekwisha tangaza Wenyeviti tuzingatie Miswada hiyo na kwa sababu hiyo hakutakuwa na shughuli za Bunge leo jioni. Kwa hiyo, sasa naahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 04:40 asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne,*
*Tarehe 31 Januari, 2007 saa tatu asubuhi)*